

# Ezra



# Contents



# Ezra

Koreshi Asaidia Watu Kurudi Kutoka Uhamishoni

1Katika mwaka wa kwanza wa utawala wa Koreshi mfalme wa Uajemi, ili kulitimiza neno la Bwana lililosemwa na nabii Yeremia, Bwana aliusukuma moyo wa Koreshi mfalme wa Uajemi kutangaza katika himaya yake yote kwa maandishi: <sup>2</sup> “Hili ndilo asemalo Koreshi mfalme wa Uajemi: “Bwana, Mungu wa mbinguni, amenipa falme zote duniani, na ameniagiza kumjengea Hekalu huko Yerusalemu katika Yuda. <sup>3</sup> Yeyote wa watu wake miongoni mweni, Mungu wake na awe pamoja naye, wacha apande kwenda Yerusalemu katika Yuda na kujenga Hekalu la Bwana, Mungu wa Israeli, Mungu aliyeko huko Yerusalemu. <sup>4</sup> Nao watu wa mahali popote wale walionusurika wanapoishi sasa, watu hao wampe fedha na dhahabu, pamoja na vifaa na mifugo, mbali na sadaka za hiari kwa ajili ya Hekalu la Mungu huko Yerusalemu.’”

5Kisha viongozi wa jamaa ya Yuda na Benyamini na makuhani na Walawi kila mmoja ambaye moyo wake ulisukumwa na Mungu, akajiandaa kupanda ili kuijenga nyumba ya Bwana huko Yerusalemu. <sup>6</sup> Majirani zao wote wakawasaidia vyombo vya fedha na dhahabu, pamoja na vifaa na mifugo, pia na zawadi za thamani, pamoja na sadaka zote za hiari. <sup>7</sup> Zaidi ya hayo, Mfalme Koreshi akavitoe vyombo vilivyokuwa mali ya Hekalu la Bwana, ambavyo Nebukadneza alikuwa amevichukua kutoka Yerusalemu na kuviweka katika hekalu la mungu wake. <sup>8</sup> Koreshi mfalme wa Uajemi akavitoe kwa mkono wa Mithredathi mtunza hazina, aliyevihasabu mbele ya Sheshbaza mkuu wa Yuda.

9Hii ilikuwa ndio orodha ya vifaa: <sup>10</sup> mabakuli ya dhahabu yalikuwa 30

11Kwa ujumla, kulikuwa na vyombo 5,400 vya dhahabu na vya fedha. Sheshbaza akavileta hivi vyote wakati watu walipotoka uhamishoni Babeli kwenda Yerusalemu.

Orodha Ya Watu Waliorudi Kutoka Uhamishoni  
(Nehemia 7:4-73)

**2** Basi hawa ndio watu wa jimbo waliotoka uhamishoni, ambao Nebukadneza mfalme wa Babeli alikuwa amewachukua mateka hadi Babeli (walirudi Yerusalemu na Yuda, kila mmoja kwenye mji wake, <sup>2</sup> wakiwa wamefuatana na Zerubabeli, Yeshua, Nehemia, Seraya, Reelaya, Mordekai, Bilshani, Mispari, Bigwai, Rehumu na Baana): Orodha ya wanaume kati ya watu wa Israeli ilikuwa: <sup>3</sup> wazao wa Paroshi 2,172 <sup>4</sup> wazao wa Shefatia 372 <sup>5</sup> wazao wa Ara 775 <sup>6</sup> wazao wa Pahath-Moabu (wa jamaa ya Yeshua na Yoabu) 2,812 <sup>7</sup> wazao wa Elamu 1,254 <sup>8</sup> wazao wa Zatu 945 <sup>9</sup> wazao wa Zakai 760 <sup>10</sup> wazao wa Bani 642 <sup>11</sup> wazao wa Bebai 623 <sup>12</sup> wazao wa Azgadi 1,222 <sup>13</sup> wazao wa Adonikamu 666 <sup>14</sup> wazao wa